
Jarida la

# SIHA NA MAENDELEO

UTAWALA BORA

www.sihadc.go.tz | Mwezi Desemba 2023 | Toleo la 12 | Halmashauri ya Siha



*Haliuzwi*

# DKT MOLLEL AKABIDHI GARI NA VIFAA TIBA VYA ZAIDI YA MILIONI 900 HOSPITALI YA WILAYA YA SIHA



*Naibu Waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Siha Mhe. Dkt Godwin Mollel akimkabidhi ufunguo wa gari la Mganga Mkuu wa Wilaya ya Siha Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka kama ishara ya kuikabidhi rasmi gari hiyo ili isaidie kuboresha huduma za afya kwa wananchi wa Wilaya ya Siha.*

Naibu Waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Siha Mhe. Dkt Godwin Mollel akabidhi Gari na Vifaa Tiba vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi Milioni 900 katika Hospitali ya Wilaya ya Siha kwa lengo la kuendelea kuboresha huduma za afya zinazotolewa na Serikali ya Tanzania kwa wananchi na Wakazi wa Wilaya ya Siha.

Mhe. Dkt mollel amekabidhi vifaa hivyo desemba 21, 2023 baada ya ufunguzi wa huduma za matibabu vipimo na matibabu ya magonjwa ya moyo yaliyotolewa na Taasisi ya moyo Jakaya Kikwete huku akiongeza kuwa baada ya kukabidhi gari hilo bado magari mawili ya wagonjwa (ambulance) ambazo zinafanyiwa maboresho ili ziwe hospitali inayotembea.

“Tulizuia hayo mawili kwa sababu tulipoangalia ndani tukagundua kuna vifaa vinakosekana, sisi hatutaki gari la kubebea wagonjwa, tunataka hospitali inayotembea ya kubebea WanaSiha wafike Mawenzi, KCMC na popote wakiwa salama” amesema Naibu Waziri Mhe. Dkt Mollel.

“Inatakiwa mtu akibebwa kwenye gari, hilo gari lenyewe liwe Hospitali kwa hiyo Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan ametupa maelekezo mahsusi Ambulance zote 889 ziwe hosptali inayotembea ili mtu akiwa njiani kama hawezi kupumua apate oksijeni ndani ya gari” ameongeza Mhe Dkt. Mollel.





*Gari la Mganga Mkuu wa Wilaya ya Siha na Baadhi ya Vifaa Tiba vyenye thamani ya zaidi ya Milioni 900 vilivyokabidhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Siha na Naibu Waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Siha Mhe. Dkt Godwin Mollel kwa lengo la kuendelea kuboresha huduma za afya zinazotolewa kwa Wananchi na Wakazi wa Wilaya ya Siha.*






*Naibu Waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Siha Mhe Dkt Godwin Mollel akizungumza na wananchi na wakazi wa Wilaya ya Siha baada ya kukabidhi Gari na Vifaa Tiba vyenye thamani ya zaidi ya Milioni 900 kwenye Hospitali ya Wilaya ya Siha.*





*Naibu waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Siha Mhe. Dkt Godwin Mollel akiwasikiliza Madaktari bingwa kutoka Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) baada ya ufunguzi wa huduma za vipimo na matibabu ya magonjwa ya moyo yaliyokuwa yakitolewa na taasisi hiyo katika Hospitali ya Wilaya ya Siha kuanzia Desemba 18, 2023 hadi Desemba 24, 2023*






*Wataalamu wa afya kutoka Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) wakitoa huduma za vipimo na ushauri wa masuala ya Lishe kwa wananchi wa Wilaya ya Siha waliojitokeza kufanyiwa vipimo na matibabu ya magonjwa ya moyo kwenye Hospitali ya Wilaya ya Siha kuanzia Desemba 18 hadi Desemba 24, 2023*





*Baadhi ya Wananchi wa Wilaya ya Siha waliojitokeza kupata huduma za kibingwa za Vipimo na Matibabu ya Magonjwa ya moyo yaliyokuwa yakitolewa na Madaktari Bingwa kutoka Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kuanzia Desemba 18, 2023 hadi Desemba 24, 2023 katika Hospitali ya Wilaya ya Siha*

## DKT. TIMBUKA AWAONGOZA WANANCHI WILAYA YA SIHA KUADHIMISHA MIAKA 62 YA UHURU




*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka akitoa hotuba ya kufunga kongamano la Maadhimisho ya Miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania Bara lililofanyika Kiwilaya katika Ukumbi wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha Desemba 09, 2023*

Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka amesema Wilaya ya Siha imepiga hatua kubwa ya maendeleo kwenye Sekta ya Afya, Elimu, Miundombinu ya Barabara, Maendeleo ya Jamii, Kilimo na Mifugo, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Sekta ya Maji.

Mhe. Dkt Timbuka amesema hayo Desemba 09, 2023 wakati akitoa hotuba ya kufunga kongamano la Maadhimisho ya Miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania Bara ambapo amesema wakati nchi inapata Uhuru Wilaya ya Siha ilikuwa na Shule Tano za Msingi na Shule moja ya Sekondari hadi Novemba 2023 Wilaya imefikisha Shule za Msingi 75 na Shule za Sekondari 22.

Amesema wakati nchi inapata Uhuru Miaka 62 iliyopita Wilaya ya Siha haikuwa na Shule hata moja ya yenye Kidato cha Tano na Sita lakini kwa sasa kuna jumla ya Shule Tisa za Kidato cha Tano na sita zinazotoa elimu kwa vijana wa wilaya ya siha na taifa kwa ujumla.

Aidha, Mhe Dkt Timbuka amesema kabla ya Uhuru hakukawa na miundombinu ya barabara iliyokuwa ikiunganisha Miji na Vijiji lakini kwa sasa barabara zinapitika wakati wote hali inayochochea upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi katika sekta ya biashara ya usafirishaji wa mazao ya kilimo.

Katika sekta ya maji mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe Dkt Christopher Timbuka amesema Serikali inaendelea kupanua na kuboresha miundombinu ya maji ili kuhakikishia wananchi huduma hiyo muhimu bila kikwazo.









*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka ( katikati mbele) pamoja na Viongozi mbalimbali wa Serikali, Kamati ya Ulinzi na Usalama, Viongozi wa Vyama vya Siasa na Viongozi wa Dini wakati na baada ya Kongamano la Maadhimisho ya Miaka 62 ya Uhuru yaliyofanyika Desemba 09, 2023 kwenye Ukumbi wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha.*





*Baadhi ya washiriki wa Kongamano la Maadhimisho ya Miaka 62 ya Uhuru yaliyofanyika Desemba 09, 2023 kwenye Ukumbi wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha.*



*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe Dkt Christopher Timbuka akifungua zoezi la upandaji miti kuzunguka eneo la makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha katika maadhimisho ya miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania Bara Desemba 09, 2023*



*Mhe. Duncan Urassa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha akishiriki zoezi la kupanda miti katika maadhimisho ya miaka 62 ya Uhuru.*



*Baadhi ya Viongozi wa Dini Wilaya ya Siha wakishiriki zoezi la upandaji miti katika eneo la Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha siku ya Maadhimisho ya Miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania Bara Desemba 09, 2023.*

## TAKUKURU WILAYA YA SIHA YATOA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA UMMA




*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Haji M. Mnasi (PhD) akifungua mafunzo kwa Watumishi wa Umma yaliyotolewa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Desemba 01, 2023 kuhusu umuhimu wa kuzingatia kanuni, taratibu na miongozo wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo*

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Haji M. Mnasi (PhD) amewaelekeza Wakuu wa Divisheni ya Elimu Msingi na Sekondari, Maafisa Manunuzi, Wahandisi, Wakuu wa Shule, Walimu Wakuu na Waganga Wafawidhi kufuata kanuni, taratibu na miongozo wakati wote wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili ikamilike kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

Mnasi (PhD) ametoa rai hiyo Desemba 01, 2022 wakati akifungua mafunzo maalum ya Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Siha na watumishi wa umma yaliyofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha.

Amesema usimamaizi wa miradi unaanzia kwenye hatua ya uchaguzi wa mafundi wanaoaminika na wenye uwezo wa kutekeleza miradi husika kwa ufanisi, kisha hatua ya manunuzi ya vifaa vya ujenzi na kuvisimamia vikamilishe kazi husika.

“Halmashauri itaendelea kutoa elimu ya namna ya kusimamia shughuli za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wahusika kadri inavyohitajika ikiwa ni pamoja na hatua za manunuzi, ushindanishaji wa mafundi, utunzaji wa rekodi za vifaa na ubora wa miradi inayotekelezwa” amesema Mnasi.



*Afisa Mchunguzi  wa Taasisi ya Kuzuia  na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Siha ndugu Yohana Marwerwe (kwanza kulia) akitoa somo  wakati wa mafunzo kwa watumishi wa umma Desemba 01, 2023 yaliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha.*





*Washiriki waliohudhuria mafunzo yaliyotolewa na Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Siha Desemba 01, 2023*

# DC SIHA AHIMIZA UTUNZAJI WA MAZINGIRA



*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe.Dkt Christopher Timbuka (mbele) akiwa amebeba miti wakati wa zoezi la upandaji miti zaidi ya 500 katika shule Mpya ya Sekondari Ormelili iliyotolewa na Benki ya CRDB ili kuendelea kutunza mazingira Desemba 13, 2023*

Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka ameishukuru Benki ya CRDB Tawi la Siha kwa kufadhili upatikanaji wa miti Zaidi ya 500 iliyopandwa katika Shule Mpya ya Sekondari Ormelili iliyojengwa kwa fedha kutoka Serikali Kuu Shilingi Milioni **584.2** ili kuboresha upatikanaji wa elimu kwa watoto wa Kata ya Ormelili waliokuwa wakitembea zaidi ya kilomita 20 kupata elimu Sekondari.

Mhe. Dkt Timbuka ametoa shukrani hizo Desemba 13, 2023 baada ya shughuli ya upandaji miti iliyotolewa na Benki ya CRDB Tawi la Siha ambapo amesema miti hiyo itachangia kwa kiasi kikubwa utunzaji wa mazingira yanayoizunguka shule hiyo na maeneo jirani.

Amesema Serikali itaendelea kushirikiana na Taasisi hiyo ili kuwaletea maendeleo wananchi na wakazi wa Wilaya ya Siha.

"Mnaweza kuona ufadhili mlioutoa ni kidogo lakini mmechangia pakubwa mno ukiangalia mazingira yanayoizunguka shule hii ya Ormelili yalikuwa na uwazi sana sasa miti hii tuliyopanda itasaidia kutunza mazingira na kuleta kivuli na utulivu shuleni, kwa hiyo tunawashukuru sana" amesema Mhe Dkt Timbuka.

"Sisi upande wa Serikali tutaendeleza ushirikiano wa karibu na Benki ya CRDB ili kwa pamoja tutoe huduma kwa ufanisi na bora kwa wananchi na wakazi wa Wilaya ya Siha na kuwaletea maendeleo" ameongeza Dkt Timbuka




**Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt. Christopher Timbuka akimwagilia mti baada ya zoezi la upandaji miti katika shule mpya ya Sekondari Ormelili**




*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Haji Mnasi, PhD (kwanza kushoto) akiwa katika zoezi la upandaji miti iliyotolewa na Benki ya CRDB Tawi la Siha katika Shule mpya ya Sekondari Ormelili Desemba 13, 2023*

# HABARI PICHA ZA MIRADI YA MAENDELEO WILAYA YA SIHA







*Muonekano wa Shule mpya ya Sekondari Ormelili iliyotekelezwa kwa Fedha Shilingi Milioni 584.2 kutoka Serikali Kuu katika Kijiji cha Ormelili, Kata ya Ormelili Wilaya ya Siha, kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi waliokuwa wakitembea umbali za zaidi ya kilomita 20 kwenda shule ya Sekondari Sikirari iliyopo Kata ya Donyomurwak, Shule hii imefunguliwa rasmi mwezi Januari,2024*



*Muonekano wa Vyumba Vinne vya Madarasa katika shule ya Awali na Msingi Mawasiliano Kata ya Gararagua yaliyotekelezwa na Serikali kupitia  mradi wa BOOST kwa fedha shilingi Milioni 106.3 ambazo zilifanikisha ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na matundu matatu ya vyoo na Pia Serikali imeongeza shingi Milioni 12.5 kwa ajili ya ukamilishwaji wa Chumba kimoja cha darasa.*

## FURSA ZA UTALII KATIKA WILAYA YA SIHA MKOA WA KILIMANJARO










*Maporomoko ya West Kilimanjaro, Fahari ya Wilaya ya Siha Mkoa wa Kilimanjaro na Tanzania kwa ujumla*

















**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha**
**5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha**
**Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677**
**Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz**

**Tunapatikana**